

## **KUOGA (JOSHO)**

Kuoga ni kueneza maji mwili mzima kwa nia ya kujitwahaisha, ni lazima katika kuoga ni kuwusha mwili wote pamoja na kusukutuwa na kuingiza maji puani.

### **MAMBO MATANO AMBAYO NI WAJIBU KUOGA.**

1. Kutokwa na manii kwa njia ya ladha akiwa macho au akiwa usingizini kwa mwanamume au mwanamke, yatakapo toka manii bila ya matamano kama vile yakitoka kwa sababu ya ugonjwa, au baridi kali hapaswi mtu kuoga, hivyo hivyo atakapoota na asipate manii au athari ya manii haitamposa kuoga pia, akipata manii au athari ya manii atawajibika kuoga hata kama hakumbuki kuwa aliota.
2. Kukutana kwa tupu mbili ya mwanamke na mwanamume kwa kuzamisha kichwa cha dhakari kwenye tupu ya mwanamke hata kama hayajatoka manii.
3. Kumalizika kwa hedhi na nifasi.
4. Mauti (kifo) ni wajibu maiti kuoshwa.
5. Atakapo silimu kafiri kuingia kwenye uislamu.

### **MAMBO AMBAYO NI HARAMU KWA MWENYE JANABA.**

Janaba ni neno ambalo linasifika kwa mwanamume na mwanamke pale wawili hawa watakapofanya tendo la ndoa, au kutoka na manii kwa matamano bila ya tendo la ndoa au kutokwa na minii kwa sababu ya kuota. Ni haramu kwa aliyepatwa na janaba;

1. Kuswali
2. Kutufu Al ka'aba
3. Kuugusa msahafu bila ya kizuizi, vile vile kuisoma Quran kwa siri au kwa wazi wazi, kwa hifidhi au kuisoma kawaida kwenye msahafu
4. Kukaa msikiti, ama kupita kwenye msikiti hakuna tatizo, na inafaa kukaa msikitini akihijia kufanya hivyo, na itahafifisha kwa kutawadha.